## KUANZISHWA KWA RUWASA

Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*Rural Water Supply and Sanitation Agency–RUWASA*) ni taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019. Jukumu kuu la RUWASA ni kujenga skimu za maji na kusimamia utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

RUWASA ilianza rasmi utekelezaji wa majukumu yake tarehe 1 Julai 2019 na inafanya kazi kwenye Wilaya 128 na Mikoa 25 ya Tanzania Bara isipokuwa Mkoa wa Dar es Salaam ambao unahudumiwa na DAWASA. Makao Makuu ya RUWASA yapo Jijini Dodoma.

## UTOAJI WA HUDUMA VIJIJINI CHINI YA RUWASA

Katika utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini, RUWASA inafanya kazi kupitia Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (*Community Based Water Supply Organisation – CBWSOs*) ambavyo vinasajiliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 32 (1) cha Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na.5 ya mwaka 2019. CBWSOs ni taasisi zilizoundwa kisheria ambazo zinajitegemea katika uendeshaji wake na zina mamlaka ya kushtaki na kushtakiwa. CBWSOs zina jukumu la kuendesha skimu za maji na kutoa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini. Pia, zina wajibu wa kuendesha na kukarabati miradi ya maji, kutegemeana na uwezo wao wa kiufundi na kifedha.

## KABLA YA KUANZISHWA KWA RUWASA

Awali, majukumu ya RUWASA yalikuwa yanatekelezwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa (RSs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Majukumu hayo ni pamoja na kuhakikisha huduma za maji zinapatikana kwenye jamii za watu waishio maeneo ya vijijini, miji midogo na makao makuu ya wilaya.

Baada ya majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa (RSs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhamishwa kwenda RUWASA, uwajibikaji wa Maafisa waliokuwa wanahusika na utoaji wa huduma ya maji ulihamishwa kwenda Wizara ya Maji kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019.

## MUUNDO WA KIUTAWALA WA RUWASA

**Kwanza,** Usimamizi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini unaanzia kwa Waziri Mwenye Dhamana ya Sekta






ya Maji, ambayo pamoja na mambo mengine, ana jukumu la kutekeleza sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali katika kufanikisha miradi na huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

**Pili,** RUWASA ina Bodi ya Wakurugenzi yenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu na utendaji wote juu ya masuala ya huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini pamoja na kumshauri Waziri mwenye dhamana kuhusu masuala yoyote yanayohusiana na huduma ya maji vijijini.

**Tatu,** Menejimenti ya RUWASA inafanya shughuli zake za kila siku kupitia ofisi zake zilizopo katika ngazi ya Mkoa na Wilaya. Hii ni tofauti na muundo wa awali ambao ulikuwa unajumuisha ofisi katika ngazi ya Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa.

Meneja wa RUWASA Mkoa ana jukumu la kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji pamoja na huduma za maji na usafi wa mazingira katika mkoa wake. Vilevile, Meneja Wilaya ana jukumu la kutoa msaada wa kiufundi kwa wilaya husika. Meneja wa Wilaya, yeye ni mtekelezaji mkuu wa miradi ya usambazaji maji na usafi wa mazingira katika wilaya yake na pia ana jukumu la msingi la kuwezesha Vyombo vya Usimamizi wa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) kuendeleza utoaji wa huduma.

### Dira

Kuwa na jamii ya wananchi waishio vijijini inayopata huduma ya majisafi na salama ya kutosha na ya uhakika pamoja na huduma ya usafi wa mazingira.

### Dhamira

Kutoa huduma ya majisafi na salama na kuhamasisha usafi wa mazingira kwa jamii iishio vijijini kwa kufanya usanifu, ujenzi, kusaidia uendeshaji wa matengenezo ya miundombinu na utoaji wa huduma kwa ajili ya kuboresha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

### Tunu

Katika kutimiza matarajio ya wateja wake, RUWASA inahakikisha kuwa watumishi wake wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia tunu zifuatazo:-

(a) Uadilifu,
(b) Ubunifu,
(c) Huduma bora,
(d) Ushirikiano na
(e) Weledi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 43 cha Sheria ya Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Namba 5 ya mwaka 2019, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ina wajibu wa kuendeleza miundombinu ya maji kwa kufanya ujenzi na usimamizi wa ujenzi wa miradi ya maji na pia kusimamia utoaji wa huduma endelevu za maji na usafi wa mazingira vijijini.

## MAJUKUMU YA RUWASA

- Kuandaa mipango, kusanifu miradi ya maji, kujenga na kusimamia uandeshaji wa skimu za maji vijijini.
- Kuendeleza vyanzo vya maji kwa kufanya utafiti wa maji

chini ya ardhi na kuchimba visima pamoja na kujenga mabwawa.

- Kufanya matengenezo makubwa ya miundombinu ya maji vijijini.
- Kusajili,kuratibu, kudhibiti, kufuatilia na kutathmini vyombo vya kijamii vinavyohusika (CBWSOs) ili kuhakikisha kuwa huduma inakuwa endelevu.
- Kuzijengea uwezo CBWSOs kwa kutoa mafunzo na utaalamu wa uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji vijijini.
- Kuhamasisha jamii na kutoa elimu ya usafi wa mazingira katika ngazi ya kaya na mtu binafsi (*sanitation and hygiene*) na masuala ya uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji.
- Inatafuta fedha kwa ajili ya uendeshaji ili kuwezesha RUWASA kutekeleza majukumu yake na kushirikiana na wadau mbalimbali katika masuala yanayohusu utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini.

## MAFANIKIO YA RUWASA

Katika kipindi cha miaka miwili, RUWASA imepata mafanikio yafuatayo:-

- Kukamilisha ujenzi wa miradi 126 kati ya miradi 177 iliyokuwa na changamoto ya utoaji huduma.
- Kukamilisha miradi 566 kati ya miradi 631 iliyopokelewa kutoka Halmashauri.
- Kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka 64.8% Juni 2019 hadi kufikia 72.3% Juni 2021.
- Kuongezeka kwa fedha za nje za utekelezaji wa miradi kutoka Sh. 29,668,865,000 mwaka 2019 hadi kufikia Sh. 265,232,166,614 Juni 2021 kutokana na ufanisi wa ujenzi miradi;
- Kuunda Mfumo wa Kusimamia Shughuli za RUWASA na Usimamizi wa Huduma – (*RUWASA Service Delivery Management System - RSDMS*) ili kuboresha ukusanyaji na upatikanaji wa wakati wa taarifa sahihi.

## HALI HALISI YA HUDUMA YA MAJI VIJIJINI

Hadi kufikia Juni 2021 idadi ya vijiji vinavyopata huduma ya maji imeongezeka na kufikia 8,348 ikilinganishwa na vijiji 7,082 vilivyokuwa vinapata ya huduma ya maji hadi Juni 2020. Huduma inapatikana kupitia vituo vya kuchotea maji 127,377 na maunganisho majumbani 157,201. Inakadiriwa kuwa, Huduma ya maji inatolewa kwa wastani wa 72.3% ya wananchi waishio vijijini, kufikia Juni 2021.



## MWELEKEO WA RUWASA

Katika kuboresha utoaji wa huduma endelevu ya maji vijijini, RUWASA inatekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo:-

- Kusanifu miradi ya maji ambayo itatumia chanzo kimoja cha maji kitakachohudumia vijijini zaidi ya kimoja na kusimamiwa na chombo kimoja ili kukidhi gharama za uendeshaji.
- Kupunguza gharama za uendeshaji kwa kutumia nishati ya umemejua na kubadilisha mitambo inayotumia dizeli na kuweka umeme wa TANESCO.
- Kuongeza usimamizi wa mauzo na makusanyo kwa kufunga dira za malipo kabla ya matumizi na kuweka mfumo wa ankra unaojulikana kama *Unified billing System* na kujiunga kwenye mfumo wa makusanyo wa Serikali GePG.
- Kuzijengea uwezo CBWSOs ili ziweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ufanisi.
- Kuwajengea uwezo watumishi kwa kuanzisha Kituo cha Mafunzo kwa Vitendo kwa Watumishi wa RUWASA (*Learning Hub*).
- Kuanzisha Kituo cha Kupokelea na Kushughulikia Kero au Malalamiko ya Wadau (*Call Centre*).
- Kuboresha usahihi wa takwimu kupitia RSDMS, ambapo katika Awamu ya Pili utaundwa mfumo wa kutumia simu za mkononi kupata taarifa zitakazokuwa zinaingizwa moja kwa moja na CBWSOs.


**Wasiliana nasi**
Jengo la Benki ya NBC, Tawi la Mazengo,
Barabara ya Kuu, S. L. P 412, 40473 Dodoma,
**Simu:** +255 (0) 2323563/4,
**Tovuti:** www.ruwasa.go.tz,
**Baruapepe:** dg@ruwasa.go.tz


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Wizara ya Maji**

RUWASA
Rural Water Supply and Sanitation Agency

# WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI



# "Maji Bombani"

